

# ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

## Marejeo ya 2015

**ATD Dunia ya Nne Tanzania**
Registration nº 003447 under NGO Act, 2002
P.O. Box 61786, Dar es Salaam – Tanzania
atd.tanzania@gmail.com
Kiingereza website: **http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/**
Kiswahili website: **http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/**

# UTANGULIZI

Mwaka 2015 haujapita sana. Mapitio haya ni mwaliko wa kukumbuka nyakati nzuri za nyuma za kushiriki, matukio, kukutana na kila mwanachama wa ATD Dunia ya Nne kama ilivyokuwa kwa mwaka uliopita.

Ni fursa ya kuweka wazi mafanikio yetu. Kwa mfano mwaka uliopita tarehe 17 Oktoba, katika Siku ya Kimataifa ya Kuushinda Umaskini Uliokithiri ambapo tulikuwa mamia kwa mamia ya watu kuonesha lengo moja la kujitoa katika kuupiga vita umaskini uliokithiri.

Watu wazima waliweza kuendelea katika kusoma na kuandika, wazazi waliweza kupata vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wao ili kuhakikisha wanapata nafasi ya kuwapeleka shuleni, kundi la wanachama ATD Dunia ya Nne walishiriki katika utafiti mkubwa kuhusu elimu.

Hata hivyo tunafahamu changamoto ambazo familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri wanakabiliana nazo lakini mafanikio yote tuliyopata yanatoa matumaini kwa dunia ambapo kila mtu anaweza kuishi kwa amani na heshima.




Tarehe 17 Oktoba
Siku ya
kuutokomeza
umaskini
uliokithiri duniani

# Je, Wote kwa pamoja katika Utu (ATD) ni nini kwa maneno machache?

"Wote kwa Pamoja" inamaanisha umoja wa Harakati, vile vile umuhimu wa kuunganisha juhudi ya kila mtu kufikia malengo husika.

"Utu" unawakilisha msingi wa harakati za ATD. Wanachama wa ATD wanaoishi katika Umaskini uliokithiri  na marafiki wanaeleza kwamba Utu unahusu thamani ya kila binadamu, pamoja na heshima ambayo kila mtu anastahili. Utu unawakilisha kiini cha ubinadamu; kila mtu ana utu. Hata hivyo, katika kesi nyingi, binadamu hawaheshimiwi kama vile invyostahili.

ATD Dunia ya Nne ni harakati za kimataifa zilizoanzishwa nchini Ufaransa mwaka 1957. Sasa ipo katika nchi zaidi ya 30 duniani kote. ATD Dunia ya Nne imekuwapo Tanzania tangu mwaka 1999 jijini Dar es Salaam: Tandale, Tegeta (Kunduchi, Boko), Chasimba na Soko la Samaki Magogoni.

Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri ni lengo kuu la Harakati zetu, kushiriki kikamilifu katika ufumbuzi wa kuondokana na umaskini uliokithiri, pamoja tunasimamia haki za wote, kujenga uelewa kwa umma na ushawishi katika sera za umma.



# ATD Tanzania mwaka 2015

## Nini utakipata katika tathmini hii?

ATD Dunia ya Nne ni harakati ambayo inakusanya watu kutoka katika asili zote ili kufikiri, kutenda, na kuishi pamoja kwa njia tofauti. Ambapo kila mtu ana nafasi ya kuchangia katika kupambana na kukomesha umaskini uliokithiri. ATD Dunia ya Nne ni harakati za watu, kila mwanachama ni mwanaharakati.

Tathmini hii inatoa mtazamo mkubwa wa matendo, matukio na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2015. Hii ni sehemu ya kwanza. Halafu unaweza kupata na kujifunza kuhusu ATD kupitia sehemu ya pili, yenye sauti na maneno ya wanachama, marafiki, wanaharakati, vijana, familia na watu wanaojitolea kwa muda wote.


**Upatikanaji wa Haki za** / Elimu Kwa Wote........................9
**Upatikanaji wa Haki za** / Cheti cha kuzaliwa..................11
**Upatikanaji wa Haki za** / Madarasa ya Elimu ya watu wazima........................................................................ 11
**Upatikanaji wa Haki za /** Kupata Shule.......................... 13
**Watoto** / Maktaba ya Mtaa.............................................. 13
**Matukio Maalum** / Mkutano nchini Kenya...................... 15
**Familia** / Kuwepo na kusaidia......................................... 15
**Vijana** / Marafiki Vijana wa ATD...................................... 17
**Matukio** / Siku ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri duniani........................................................................... 19

**Mama Mkude** -Tandale........................................ 21
**Bi Agnes** – Tegeta.................................................23
**Selemani** - Soko la Samaki...................................25
**Mheshimiwa Kasian** – Tegeta..............................27
**Yusufu** - Soko la Samaki.......................................29
**Ally Shabani** – Youth Group.................................31
**Beatrice Alperte** – ATD Dunia ya Nne rafiki........33
**Salma Mosha –** Wa kujitolea muda wote............34
**Nembo mpya ya ATD**.......................................... 35



# *Upatikanaji wa haki za*


## Upatikanaji wa Haki za Elimu kwa Wote

Elimu ya msingi ni moja ya misingi wa maisha. Haki ya mtoto kupata elimu ya msingi si kitu cha maridhiano, bila kujali familia ya mtoto kiuchumi, kiutamaduni au historia ya jamii yake. Hata hivyo, kwa watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri sana, uwezekano wa kupata na kumaliza masomo yao ya shule ya msingi umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mzazi anapoona mtoto wao ananyimwa haki za muhimu ya elimu ya msingi,  wanachojua ni kwamba umewafungia nje ya dunia yenye fursa, uwezeshwaji, na maendeleo binafsi ya hapo baadae.

Katika 2015 ATD Dunia ya Nne ilianza mradi wa utafiti shirikishi ili  kuelewa juhudi zinazofanywa na changamoto zinazowakabili wadau wa elimu ili kuhakikisha watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanaanza na kumaliza elimu yao ya msingi. Kikundi cha utafiti chenye wanachama wa ATD kutoka asili mbalimbali kiliundwa ili kuongoza mradi huu. Kikundi ambacho kilijumuisha walimu, watu wanaoishi katika umaskini na wafanyakazi kudumu wa kujitolea wa ATD, walipata mafunzo ya kutoa kipaumbele kwa kutumia uzoefu wao wa kipekee katika maisha yao kwenye utafiti huu.

Kikundi kiliwahoji, walimu, watoto, wazazi na viongozi wa serikali za mitaa ikiangalia nyumba, shule na athari kubwa kwa jamii juu ya elimu ya watoto wa shule za msingi. Utafiti huu ni endelevu na matokeo yatapatikana mwaka 2016.





## *Upatikanaji wa haki za*

## Cheti cha kuzaliwa

Watoto Sabini na nne kutoka familia sitini na saba kutoka Tandale, Tegeta na Chasimba walisajiliwa kupata vyeti vya kuzaliwa, moja ya haki muhimu kwa mtu yeyote. Mtoto anakuwa raia anayetambulika kisheria.

Hii isingewezekana bila kujitolea kwa watu kutoka katika jamii husika kwa mfano Venance, Shabani na Baba Meresiana kutumia muda na nguvu katika kuandaa mchakato, kusaidia familia kwenda RITA na mamlaka ya umma ya kusimamia mchakato wa kupata cheti cha kuzaliwa.

Baba Mericiana anasema: "*Ninachoelewa ni kwamba mradi huu unashughulikia zaidi familia maskini. Hiki ni kitu ambacho naweza kufanya kwa ajili ya watu walio katika hali sawa na mimi*".

Mradi Usajili wa Vyeti vya kuzaliwa unafadhiliwa na Hilfe für Afrika na Diplomatic Spouses Group.

## *Upatikanaji wa haki za*

## Madarasa la Watu wazima

Mradi wa Elimu ya Watu wazima uliendeshwa Tegeta mwaka 2015. Katika kipindi hiki watu kumi na saba walianza darasa na kuhudhuria mara kwa mara kwa miezi mitatu ya mwanzo. Bwana Kasian na na mke wake Bi Agnes, walisaidia sana mradi huu kwa wiki ya kwanza katika kuhamasisha watu kutokuwa na hofu na kujiamini wenyewe.
Bwana Kasian, alitoa msaada usio rasmi kwa watu wa jamii yake kutaka kujifunza kusoma na kuandika kabla ya darasa kuanza. Alitekeleza mradi na ATD Dunia ya Nne katika kukabiliana na mahitaji ya jamii yake.
Kwa sababu ya ugumu wa maisha baadhi ya watu walikuwa wakiondoka darasani lakini wale ambao walifanikiwa walijivuna: "*Kabla nilikuwa mwenye aibu sana kuomba kuelekezwa mji, sikuwa na uwezo wa kusoma alama za barabarani. Lakini sasa najisikia huru kutembea na kuwasiliana na familia yangu kupitia simu yangu, sina aibu tena*".





## *Upatikanaji wa haki za*

## Haki ya Kwenda Shule

Mwaka 2015, ATD iliwasaidia watoto maskini sana kupata elimu ya msingi na sekondari.

Upatikanaji ulikuwa wa uhakika kwa kupata vyeti vya kuzaliwa, kusaidiwa kujiandikisha shuleni, kusindikizwa kwa familia katika kukutana na walimu wakuu wakati matatizo, nk.

Kupata elimu ni moja ya haki muhimu kwa binadamu na ni moja ya njia bora ya kuondokana na umaskini. Zaidi ya maarifa, ujuzi na ushindani, ni njia ya kuelewa masuala mbalimbali ya maisha, kuchanganyika na aina mbalimbali za watu, ili kupata kujiamini, na kwa mtoto kupata nafasi yake mwenyewe katika jumuiya na jamii.

## *Watoto*

## Maktaba ya Mtaa

Kila Jumatano mchana wanachama wa ATD Dunia ya Nne huleta vitabu, magazeti na penseli katika Maktaba ya Mtaa huko Tandale. Wastani wa watoto 50, wenye umri wa miaka 3-10, hushiriki katika shughuli hizi: kusoma, kuimba, kucheza, kuchora.

Timu hukaa katika eneo nje na kukaribisha watoto kusoma vitabu, kusikiliza hadithi, kuandika au kuchora. Na inatoa watoto nafasi ya kujifunza, kufungua akili zao na kubadilishana mawazo. Kupitia Maktaba ya mtaa, wanachama wa ATD pia hujenga uhusiano na familia na kufahamu kuhusu masuala yanayoikabili jamii.





## Matukio Maalum

### Mkutano nchini Kenya

Wawakilishi watatu walikwenda kukutana na marafiki nchini Kenya. Venance, anayewakilisha familia za kitanzania na Salehe na Rachel, kutoka katika timu ATD Dunia ya Nne Tanzania.

Venance alituambia: "*Tulikutana na wasomi, wanafunzi, wanaharakati na familia huko Nairobi. Ilikuwa ni fursa ya kuiwakilisha ATD Dunia ya Nne na kile tunachokifanya hapa jijini Dar es Salaam. Tuliweza kupajua Kibera, eneo kubwa linaloonekana ni la kimaskini ambapo tuliona mapambano ya watu, wazazi, vyama kupata shule na huduma za afya.*

*Safari hiyo ni fursa ya kujifunza kutoka kwa kila mmoja, kama tuliona jinsi mshikamano wenye nguvu ulivyo muhimu katika kuondokana na umaskini, na hakuna kitakachofanyika bila ya kuwa na uhusiano mzuri kati ya watu.*"

## Familia

### Uwepo na msaada

ATD Fourth World members take the time to sit and listen individually to people living in extreme poverty. This is particularly important as most of the time their voices are unheard, even if they are the ones who know better about their difficult situation. This is also part of dignity; all people have something to say and deserve to be listened to.

This is possible by creating strong links with others, visiting people and understanding deeply about their lives, sharing moments of joy, achievements and challenges in their daily struggle. Regular visits create a deep trust, families can share personal difficulties, break the loneliness caused by exclusion and build a strong solidarity with ATD Fourth World members.



## Vijana

# Marafiki Vijana wa ATD

Lengo la kikundi cha Marafiki vijana wa ATD ni kuwafikia vijana wengine wa asili mbalimbali, kujiunga pamoja nao, kubadilishana mawazo na kujifunza kutoka kwa kila mmoja. Lengo kuu la kuja kwa watu kutoka matabaka mbalimbali ni kujenga fikra yakinifu na kutomwacha mtu nyuma. Kueneza ujumbe wa ATD Dunia ya Nne na kuonyesha kwamba vijana wana hamu, dhamira na nia ya kujenga jamii yenye nguvu. Wanalenga kuondoa chuki miongoni mwa vijana kwa kuonyesha kwamba matendo yao ni ya thamani na yana maana.

Kwa mwaka 2015 Vijana marafiki wa ATD waliwezesha uendeshaji wa maktaba ya Tandale kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi. Katika eneo ambalo vijana wanalaumiwa kwa kiasi kikubwa katika kuporomoka kwa maadili kwenye jamii ni uhalifu, hii ni makisio chanya kwa ajili ya watoto na wazazi kuona nia ya vijana katika kujitolea kuleta amani na kujenga urafiki.

Marafiki vijana wa ATD waliendelea kusaidiana na kukutana mara kwa mara katika ofisi za ATD, kujadili mada muhimu kama vile afya, elimu na mafunzo. Waliandaa na kuwasilisha mchezo wa kuigiza kuhusu changamoto ya kwenda na kutokwenda shule katika Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri.






17 Oktoba
Sikuya
kuutokomeza
umaskini
katika umaskini uliokithiri haki za binadamu
Kuungana pamoja ili kuhakikisha kwamba hizi
zinaheshimiwa ni jukumu letu sote,

# Matukio

## Siku ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri duniani

Oktoba 17, 2015, siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri ilisherehekewa nchini kote Tanzania, kwa namna ya pekee katika mikoa ya Dar es Salaam, Njombe na Dodoma. Mwaka huu uhamasishaji ulilenga:

**"Kujenga nyakati zijazo zilizo endelevu: Kushirikiana katika kukomesha umaskini na ubaguzi"**

Siku hii ilikuwa ni fursa ya kuwaleta pamoja wale wote ambao walidhamilia kuushinda umaskini uliokithiri kwa miaka yote na wale ambao wanaishi katika umaskini kila siku. Nia kuu ya maadhimisho ni kupaza sauti za watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kuzungumza na kushuhudia kwa niaba ya wale wasioweza kupaza sauti zao na kusikika.

Mwaka huu kamati ya Oktoba 17, ilijumuisha marafiki wa ATD Dunia ya Nne, wanaharakati wanaoishi katika jamii na wafanyakazi wa kujitolea kwa muda wote wanaotambua umuhimu wa kushiriki matukio haya na marafiki duniani kote. Walisisitiza juu ya kuchukua fursa ya kueneza ujumbe wa ATD Dunia ya Nne.

Kwenye Meza ya majadiliano mjini Njombe na marafiki wa chama cha wahunzi cha Kisangani, mkutano katika kijiji cha Bihawana (karibu na Dodoma), na mkutano mkubwa uliokusanya mamia ya watu jijini Dar es Salaam katika Kijiji cha Makumbusho ulihamasisha watu wengi.





***Mama Mkude (Tandale)***

Nina furaha sana kuhusu kile kinachofanywa na ATD mwaka huu, hasa furaha ya kushirikishwa katika mradi wa utafiti ambao bila hata kujali kiwango cha juu cha elimu au mafunzo, mimi pia niliweza kuchangia katika kazi za kitaaluma. Watu walijitoa kwa ujumla. Tulikuwa tunashughulikia baadhi ya changamoto kupitia mradi huu wa utafiti, kwa mfano baadhi ya watu tuliokutana nao walikuwa wanatarajia fedha kama mchango kwao. Lakini walibaini kuwa, pamoja na kuwa wanaishi katika umaskini, pia walikuwa na kitu cha kutoa na kushiriki na kwamba kwa kufanya hivyo wanaweza kujisaidia na kuwasaidia wengine.

Katika jamii yetu niliweza kuelewa kwamba baadhi ya njia ya huduma za kijamii hazikutolewa ipasavyo kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri: kwa mfano bado hakuna ufanisi katika upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa ajili yao, ukosefu wa taarifa, gharama za usafirishaji, rushwa n.k, Hivyo ni baadhi ya vikwazo vilivyobaki na kusababisha matatizo katika kupata Haki zao. Itakuwa vizuri kwa mamlaka husika katika kupata uelewa mzuri wa mahitaji, ATD inaweza kusaidia na kushirikisha utaalamu wake na kukabidhi yaliyofanyika kwa mamlaka husika.

Nilikwenda Dodoma kukutana na marafiki wa ATD kwa ajili ya Siku ya Kimataifa ya Kuutokomeza Umaskini Uliokithiri kwa mwaka 2015. Ilikuwa ni zaidi ya safari: hii imenisaidia kukuza ufahamu wangu na kunipa nguvu ya kusonga mbele zaidi kupitia kujitolea kwangu.  Niligundua kwamba watu wengine pia hukabiliana na changamoto kama yangu na kwamba hatuko peke yetu.



***Bi Agnes***
***(Tegeta)***



Nina furaha sana kuhudhuria siku hii ya tarehe 17 ya mwezi Oktoba. Siku hii inatarajiwa kutoa ujumbe kuhusu harakati na uelewa wa yale yanayotokea katika sekta mbalimbali za ATD Dunia ya nne. Mwaka jana niligundua kuwa hakukuwa na manufaa kwa kualika watu zaidi kutoka nje ya wanaharakati. Jamii itakuwa tofauti zaidi, tunaweza kubadilishana mawazo na kujifunza zaidi kutoka kwa wengine. Hii itasaidia harakati zetu kukua.

Kama sehemu ya darasa la elimu ya Watu wazima miaka michache iliyopita, nilipata zaidi ya nilivyotarajia: Nilijivunia kutoka kwa watu wengine na mimi mwenyewe, watu waliniona nikisoma gazeti, nilikuwa mtu! Leo mradi umepata mafanikio makubwa. Watu wa kitongoji changu huuliza maswali. Nikawa mlengwa wa ndani. Lakini wakati mwingine sijui nini cha kujibu kwa sababu nakosa habari. Ni pia vigumu kuelezea ATD Dunia ya Nne ni nini? Hivyo kwa maoni yangu, itakuwa na manufaa kwa kuhakikisha wanaharakati wa ATD wanatoa taarifa kuhusu wanayofanya ili kujenga zana zitakazo tusaidia kueleza kuhusu ATD na kushawishi watu zaidi kujiunga nasi. Mafunzo kwa kila mwanachama yataimarisha kujitoa kwetu katika harakati hizi.

Tunapaswa kutambua watu wasiohusishwa. Ni muhimu kwamba kipaumbele kiwe kinatolewa kwao katika harakati. Ni muhimu kuwaonesha kuwa hawako peke yao.





***Selemani***
***(Soko la Samaki)***

Nilipojiunga na elimu ya Watu wazima miaka michache iliyopita kwanza watu walikuwa na shauku ya kujua ni kitu gani mimi nilikuwa nikifanya. Marafiki zangu waliniunga mkono, niliweza kupata muda  wa kujifunza kusoma. Leo hii watu ambao wanataka kuwa wanafunzi huja kwangu. Kwanza mimi nilikuwa mwanafunzi, sasa mimi ni mwalimu msaidizi na natoa taarifa kwa wengine. Sasa ninapata habari na ninajua nini kinaendelea katika nchi yangu. Ninajiamini. Kusoma ni kupata maarifa.

Tarehe 17 mwezi Oktoba: ni siku ya kujivunia. Mwaka jana niliweza kushuhudia yote yanawezekana kwa kushirikishana uzoefu wangu. Ilikuwa Njombe na ilikuwa ni hatua muhimu kwangu. Uzoefu wangu ulinihamasisha kufanya juhudi zaidi ili watoto wangu wapate maisha bora. Nashukuru kupitia  ATD nimekutana na marafiki wapya, waliofungua mawazo yangu: sasa  naweza kufikia mambo ambayo yalionekana hayawezekani kwangu kabla.



***Mr. Kasian (Tegeta)***



Vitendo vilivyofanywa na harakati katika kusaidia raia kufungua macho yao na kusaidia upatikanaji wa haki zao, kwa kujivunia na kutokuwa na aibu tena. Kupata haki zao kutoka kwa polisi katika kujilinda.

Kwangu kujua kusoma na kuandika ni kitu kinachorejesha haki ya kuwa sehemu ya nchi katika kutoa mapendekezo na kuwa raia. Darasa la elimu ya watu wazima ni changamoto kubwa kwa walimu, wanapaswa kujibidiisha sana. Wakati mwingine walimu hufundisha kwa haraka sana kwa watu wazima, inaweza kuleta ugumu kwa watu wazima. Kama mwanaharakati ninahitaji kupata zaidi habari kuhusu miradi kwa wakati. Huwa napata maombi na maswali kutoka kwa watu, lakini si mara zote najua nini cha kujibu au jinsi ya kujibu.

ATD Dunia ya Nne inaweza kwenda mbali zaidi na inaweza kuongeza uelewa kwa watu wanaofanya kazi katika ngazi ya serikali. ATD Dunia ya Nne ingeweza kufanya kazi kwa karibu zaidi na serikali, kwa sababu ATD inafahamu kwa kiasi gani watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanateseka na tunaweza kuleta mawazo safi kwa serikali. Tunaweza kutoa mwelekeo na mwongozo kwa mamlaka husika.





***Yusufu***
***(Fish Market)***

Mimi niliingia ATD Dunia ya Nne karibu miaka mitatu iliyopita kupitia rafiki yangu Hassan ambaye hajui kusoma wala kuandika. Tangu mwanzo Mimi nilikuwa na msisimko katika hizi harakati, Nilijua ilikuwa muhimu kwa ajili yangu, nilitaka kuanza kushiriki kozi za kusoma na kuandika! Nilihamasika sana. Niliandaa kazi yangu kwa wakati, kwa sababu ni kipaumbele changu kwa ajili ya kujifunza. Walimu hujitoa sana.

Nina changamoto moja tu: upatikanaji wa umeme wa kufanya kazi zangu za nyumbani. Nilipata mahali pa kufanya hivyo: chini ya taa za kituo cha kuogelea. Kujifunza kusoma kumenifanya nijisikie vizuri. Kabla sikuweza kusoma ujumbe kwenye simu yangu ya mkononi, leo naweza hata kusoma magazeti. Hatua ijayo ni kujifunza Kiingereza. Darasa la kusoma na kuandika lilinihamasisha, nitajihusisha zaidi katika harakati.

Tarehe 17 mwezi Oktoba ina maana kubwa sana kwangu, Sikufikiri kamwe kuwa siku moja ningeshiriki katika aina hii ya mkutano na kubadilishana uzoefu. Sasa nimepata nafasi yangu, naweza kusimama mbele ya hadhara bila kusita. Najua kwamba nguvu na ushiriki unapokuwepo kila kitu kinawezekana. Itakuwa bora kama tunaweza kuwajulisha watu wengi iwezekanavyo, ikiwa ni pamoja na wanasiasa. Lakini nashangaa jinsi gani tunaweza kufanya hayo. Si rahisi kueleza ATD Dunia ya Nne ni nini? Tunaweza kuwa na uwanda mkubwa wa matendo yetu. Usambazaji wa kazi za utafiti utakapo kamilika mwaka huu utasaidia kuonyesha mchango wetu katika hili.

Mnamo Oktoba nilikuwa sehemu ya safari ya Dodoma. Niliweza kutambua kwamba mimi si mmoja tu katika hali yangu, na kwamba kubadilishana uzoefu wangu kungeweza kuhamasisha watu wengine.


EXCELLENT
Exercise Book




***Ally Shabani***
***(Kundi la Vijana)***

Nina umri wa miaka 20, nilipata kushiriki katika ATD mwaka 2015 namshukuru rafiki yangu mmoja wa shule. Mimi ni sehemu ya mradi wa Maktaba, uzoefu huu unanifanya nipate msukumo thabiti na kufanya kazi na watoto huleta furaha sana. Hakuna tofauti kati ya watoto.

Kupitia ATD Napata uzoefu wa kipekee na kufurahia uhusiano wa kindugu. Wazazi wa karibu hutuamini, hutuuliza kama wanaweza kuleta watoto wao. Tunafanya mambo chanya.
Oktoba 17 tulijipanga kuwakaribisha na kuwaandalia watoto warsha, kwa kucheza, kuimba, nk Tulihakikisha kwamba washiriki wote walikaa kwemye viti. Ilikuwa ni nafasi ya kuwakaribisha vijana wapya kujiunga nasi.

Tulitengeneza jukwaa la maonesho kuhusu hali halisi ya maisha yetu na maisha ya vijana wengine. Ilikuwa ni njia nzuri ya kueneza ujumbe wenye nguvu na kuishi pamoja kupitia uzoefu wa kutosha. Ilikuwa na manufaa kuongoza baadhi ya masuala ya mawasiliano kwa kuwashawishi vijana wengi zaidi kujiunga na ATD. Nina imani kwamba vijana wengi wangekuwa na furaha kujiunga na ATD Dunia ya Nne kama wangeifahamu zaidi. Vijana wa ATD Dunia ya Nne lazima kuwa wawazi zaidi.





***Beatrice Alperte***
***(ATD Dunia ya Nne rafiki)***

Nipo nchini Tanzania tangu Mei 2015, Nafanya kazi katika ubalozi wa Ufaransa jijini Dar es Salam. Mwaka 2000, nilikutana na Bi Geneviève Anthonioz-De Gaulle, aliyekuwa Rais wa ATD Dunia ya Nne huko Paris. Alialikwa na marafiki zangu ili kuwaeleza kuhusu harakati. Alijivunia sana kupaza sauti ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Alituambia kuhusu shughuli za ATD katika maeneo yao ya kazi na sauti ya wanadamu. Nilipofika Tanzania, niliamua kuchangia na kusaidia, nilifikiria juu ya historia ya ATD Dunia ya Nne na nikaamua kuwasiliana na timu. Nilichukuliwa na kufanya kazi kama "rafiki", ambayo ni hatua ya kwanza ya uhusiano. Nina furaha sana kuchangia na kuunganisha habari itakayojumuishwa katika tathmini hii ya kila mwaka. Nimekaribishwa mara nyingi na timu. Kujitolea kwa wanachama ni jambo kubwa sana. Nachukulia kuhususihwa na ATD kama ni mtazamo mpya. Naelewa vizuri athari za binadamu zinazosababishwa na umaskini na uharaka wa kubadili mambo. Hatua ni muhimu: ujinga unamaanisha kuwa nje ya maendeleo ya nchi na kuteseka, ukosefu wa cheti cha kuzaliwa humaanisha kukosa haki za msingi.

Katika kazi yangu ubalozini na mahusiano yangu na watu wa Tanzania naweza kuhusisha mambo hayo muhimu. Nikiwa ATD Dunia ya Nne nilikutana na watu wamesimamia kwa ufanisi hatua za kuboresha maisha ya watu katika umaskini uliokithiri. Kushirikiana siyosuala la fedha, kila mtu anaweza kushirikisha kitu, kulingana na uzoefu wa mtu. Nilikutana na watu wanaoishi kama "familia", kama Bi Anthonioz-De Gaulle alivyokuwa akisema.

***Salma***
***(ATD Tanzania; mfanyakazi wa kujitolea muda wote)***



Kwangu mimi, 2015 ilikuwa mwaka maalum hasa kwenye suala la maktaba. Tulitaka kila Jumatano alasiri kuwa muda wa amani, furaha na urafiki. Wakati mwingine si rahisi, watoto wanaweza kuwa na woga, kutokuwa tayari kusikiliza kwa umakini, kutokuwa tayari kushirikiana nasi kama tulivyotaka. Ninapokwenda Maktaba ya Mtaa ninakuwa na matumaini ya mabadiliko mazuri kwa watoto na jamii. Na tuliona mabadiliko. Mwaka 2015 ulidhihirisha nguvu ya Maktaba ya mtaa kusaidia watoto katika maandalizi yao kwa ajili ya shule na maisha.

Wiki baada ya wiki, watoto wadogo kwa wakubwa walikuja mara kwa mara, walikuwa huru kurudi tena na tena. Walifurahia kujifunza, kugundua mambo mapya, kufanya mazoezi katika moyo wa urafiki na kuheshimiana. Wanatuamini na wanajua jinsi gani ni muhimu na huzaa matunda kujifunza na kushiriki katika shughuli za pamoja.

Maktaba ya Mtaa huwezesha familia pia kushiriki. Wakati mwingine baadhi ya wazazi husaidia kuwakusanya watoto kwa ajili ya shughuli za Maktaba. Wakati mwingine baadhi ya wazazi kusaidia pia kuzishirikisha na familia nyingine juu ya umuhimu na thamani ya Maktaba ya mtaa. Kwa sababu licha ya kuwepo Tandale kwa miaka, kuna familia ambao bado hawajui nini tunafanya na wanahitaji kuhakikishiwa juu ya hilo.

Maktaba ya Mtaa ni zaidi ya kitu rahisi, ni kitu ambacho kinajenga mahusiano katika jamii na kutoa nguvu kwa watoto na kuwaandaa kujifunza na kuishi na watu wengine, bila kutengwa.

# NEMBO MPYA YA ATD

## Mwonekano mpya, Ujumbe uleule

As the result of a wide consultation with a diversity of members around the world, we are pleased to present our new logo.

The initial 1987 form engraved on the Commemorative Stone in Honor of Victims of Extreme Poverty situated on the Plaza of Human Rights and Liberties in Trocadero, Paris and elsewhere around the world. That logo it will remain emblematic of the conviction that links human rights defenders around the world.

ATD Fourth World's logo for 2015 onward also stays faithful to founder Joseph Wresinski's vision for a design that conveys the energy behind our movement:
**"*You see people reaching from the darkness towards the light, to catch, to hold onto the bird which symbolizes hope, love, brotherhood, as well as joy and freedom. The circle shows that everything takes place within a community, a sense of solidarity. The whole of humanity lunges forward, constantly reaching toward the horizon."***

Created by graphic designer Marie Giard, the new logo takes the powerful symbols of the past emblem — solidarity, hope, freedom — and works them into a bolder design to evoke the same spirit of striving **A**ll **T**ogether in **D**ignity to end poverty and exclusion.

In designing priorities for 2013 – 2017 (see following pages), ATD Fourth World members set a goal together to better organise for human rights and peace.

## *“Where will I be tomorrow”*

Constantly moving with no permanent settlement; worrying each day where to find food; ignored, or worse, considered without value; seeing their children not going to school; again and again struck down by sickness; thinking that in everything they try to do they fail; this is the life of the poorest people, unknowing and continually asking themselves in spite of all their efforts, *“Where will I be tomorrow?”*

And yet, as the grip of extreme poverty all but suffocates all hope from the lives of people living in extreme poverty, their resilience, aspirations, knowledge and efforts to build a world of peace can be an inspiration for humankind.

## *Ambitions*

### Valuing all Humans as Equal - Priority to the Poorest

ATD Fourth World’s priority is to go step by step, word by word, with the poorest people in all we do. In order to create meaningful and trusting relationships we will open our hearts, minds and souls to know one another sincerely and continue our search for those who are missing. We must be respectful in our search for understanding the suffering they endure each day, and encourage society to learn of the efforts and gestures they make to build stronger communities.

**Learning for Life**
The thirst for knowledge of people living in poverty of all ages is never diminished regardless of the hardships they face. We will deepen our understanding of all aspects of education and learning for life, starting at home, in the wider community, in schools and centers of further education. A priority will be to identify the efforts people living in poverty make and the barriers they face to succeed in their quest for knowledge. We must emphasis the joy of learning and encourage mutual participation and reject competition.

**Young People - Carrying our Hopes**
At the very moment in life when young people crave the freedom to express themselves, individually and collectively, they face the challenge of responsibilities being thrust upon their young shoulders. We will encourage young people from all backgrounds to express themselves and follow their dreams. It is essential their actions are recognised within their communities as building peace and carry forward the hopes of their nation.

**Creating an Inclusive World**
Our Movement, our vision, is for the world, for poor and rich, for all humans to live in unity and peace, with dignity and in a sustainable way. We will enable people to understand and access their fundamental rights. To spread our message we will share our vision, starting with our neighbours, our communities and beyond. We will develop new partnerships and create new friendships with individuals and groups and through cooperation share the knowledge, ideas and skills we have for the benefit of all.



**ATD Dunia ya Nne Tanzania**
Registration nº 003447 under NGO Act, 2002
P.O. Box 61786, Dar es Salaam – Tanzania
atd.tanzania@gmail.com
Kiingereza website : http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/
Kiswahili website : http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/

AGENCE FRANÇAISE DE DÉVELOPPEMENT